MAAMBUKIZI | Idadi imeanza kuongezeka tena nchini huku kirusi kipya Omicron kikiibua hofu duniani

# Covid sasa yatishia sherehe za Krismasi

**Katika takwimu zilizotolewa jana, jumla ya visa 853 viliripotiwa kote nchini; Nairobi, Kiambu na Nakuru zinaongoza orodha hiyo**




**Waziri wa Afya katika mojawapo ya vikao vya kutoa taarifa za punde kuhusu hali ya corona nchini, katika jumba la Afya House mjini Nairobi. Hapa aliandamana na Waziri wa Utalii Najib Balala.** PICHA | LUCY WANJIRU

NA CECIL ODONGO

**MAAMBUKIZI** ya virusi ya corona sasa yanatishia kuharibia Wakenya sherehe za Krismasi na mwaka mpya huku takwimu zinazoripotiwa na Wizara ya Afya kila siku zikiendelea kupanda kama tu hali ilivyokuwa corona ilipotua nchini mwaka jana.

Hapa jana, Wakenya 1,609 walipatikana na virusi hivyo, wakati ambapo pia kuna hofu kuwa kirusi mpya aina ya Omicron kinazidi kuenea kote nchini. Idadi hiyo ya walioambukizwa jana, ilitokana na vipimo vilivyofanyiwa sampuli 7,176 kwenye maabara ya serikali na kupandisha pia asilimia ya maambukizi hadi 22.

Idadi ya jana ilikaribia mara mbili ya ile iliripotiwa Alhamisi ambapo watu 943 walipatikana na virusi hivyo wakati ambapo serikali nayo inaendelea kuwarai raia wapate chanjo ili kupata kinga imara mwilini.

Kwa kuwa imesalia siku saba tu kabla ya sherehe za Krismasi na 12 kabla ya kuvuka mwaka, hekaheka za safari zinaendelea kunoga Wakenya wengi wakitoka mijini kuelekea mashinani ili kujiunga na jamaa na familia kwa sherehe hizo.

Aidha baada ya shule kufungwa jana, wanafunzi nao wanatarajiwa kuungana na familia zao mashambani hali inayowaweka hatari wakongwe kuambukizwa janga hilo iwapo wanaosafiri watakuwa na virusi hivyo.

Jiji la Nairobi - ambako wengi watakuwa wakiondoka kuelekea mashambani hasa maeneo ya Nyanza, Bonde la Ufa na Magharibi - linazidi kushuhudia kupanda kwa maambukizi.

Katika takwimu za jana, jumla ya visa 853 viliripotiwa kote nchini.

Kiambu ainayopakana na Nairobi ilikuwa na visa 158.

Nakuru - ambayo ilikuwa kati ya kaunti zilizofungwa hapo awali - iliandikisha visa vipya 113.

Kupanda huko kwa idadi ya maambukizi kunajiri wakati Wakenya wengi wameonekana kukosa kumakinikia vilivyo kanuni kali zilizowekwa mwanzoni mwa janga hili na serikali; zilizochangia pakubwa katika kuzuia msambao wa virusi hivyo vilivyosababisha mauti ya mamilioni kote duniani.

Katika vituo mbalimbali hasa jijini Nairobi, wasafiri wengi huwa hawavai barakoa au wakiwa nayo basi hawaivalii vizuri, wakimakinikia tu kusaka magari ya kuwasafirisha mashinani.


Ingawa mwanzoni, vingi vya vituo vya mabasi viliweka sanitaiza na maeneo ya kunawa mikono, hali sasa ni tofauti huku wahudumu hao katika sekta ya uchukuzi wakikosa kuzingatia masharti yanayohitajika.

Aidha kwa kuwa ni msimu wa siasa, kumekuwa na ongezeko la mikutano, hali ambayo pia itachangia ongezeko zaidi, wanasiasa wakilenga kuwashawishi raia wawachague mwakani.

Kuhusu chanjo, kumekuwa na hamasisho kuwa wengi wajitokeze ila hata baada ya serikali kutishia kuwa watakosa huduma muhimu za serikali, bado idadi ya wanaojitokeza ni chini.

Kufikia Jumatano, ni Wakenya 5,611,371 ambao wamepokea angalau chanjo moja huku Waziri wa Afya Mutahi Kagwe akisema wanalenga Wakenya 27,246,033.

# Usalama: Wakenya wahimizwa kuwa macho zaidi sikukuu




**Waziri wa Usalama Dkt Fred Matiang'i.** PICHA | MAKTABA

NA WYCLIFFE NYABERI

**WAZIRI** wa Usalama Dkt Fred Matiang'i amewaomba Wakenya wawe waangalifu mno kuhusu usalama wao msimu huu wa Krismasi na shamra shamra zingine za mwezi wa Desemba.

Dkt Matiang'i amedokeza licha ya serikali kuweka usalama wa kutosha kuwalinda raia, Wakenya hawafai kujisahau wala kubebwa na mahanjam ya sherehe hizo kwa kuwa adui hajulikani atakapovamia.

Waziri huyo akiongea kwenye hafla ya mazishi jana eneobunge la Nyaribari Masaba, kaunti ya Kisii, aliwatahatarisha raia hasa waishio vijijini wasidhani mashambulizi hutokea maeneo ya mijini pekee.

Alitolea mfano tukio la hivi majuzi ambapo mhanga mmoja wa kujitolea alijilipua katika eneo la Nyakach, kaunti ya Kisumu na kusema tukio hilo linafaa kuwa funzo kwao ya kwamba wanafaa kumakinika zaidi.

"Nataka kuwaambia Wakenya na watu wetu nyumbani tafadhali jitunze. Kadri tunavyozidi kuwahakikishia usalama wenu, nanyi pia msilale. Oneni tukio la Nyakach ambalo lilifanyika katika eneo nililokuwa juzi. Kaeni macho sana," Dkt Matiang'i


> "Kadri tunavyozidi kuwahakikishia usalama wenu, nanyi pia msilale."
>
> Waziri wa Usalama Dkt Matiang'i akiwa mjini Kisii

akatanabahi.

Aliomba raia kupiga ripoti kwa maafisa wa usalama kuhusu watu wowote watakaofika vijijini wasiojulikana vyema au watakaowashuku.

Dkt Matiang'i alionya wanasiasa wasiwagawanye raia kwa semi za chuki na matusi, kwani uchaguzi ni wa siku moja na huja na kuenda.

# Mzozo wa kanisa la Methodist wachacha



**Kasisi Msimamizi Joseph Ntombura (*kulia*) wa Kanisa la Methodist awali mwaka huu.** PICHA | MAKTABA

NA DAVID MUCHUI

**KANISA** la Methodist limemtimua Askofu Mkuu wa zamani Stephen Kanyaru, kuhusiana na jaribio la juzi la kutwaa uongozi wakati mkuu wake Kasisi Joseph Ntombura alikuwa nje ya nchi.

Kupitia notisi katika gazeti la ***Daily Nation*** mnamo Ijumaa, Kamati Kuu ya kanisa hilo ilisema Askofu Kanyaru - ambaye alistaafu 2013 na kumpa Kasisi Ntombura wadhifa huo - ameondolewa kama mwanachama wa kanisa.

Pia Askofu wa zamani wa Nyambene, Misheck Kanake, na Katibu Isaiah Deye pia waliangukiwa na shoka hilo la kutimuliwa kanisani.

Wengine ambao wamefurushwa ni Dkt Charles Makonde, Jacob Gituma, Maingi Rukaria, James Muriki, Ronald Nzai, Richard Yaro, Dkt Lawrence Chidongo na Cosmas Tuji.

Vilevile, washiriki ambao wamekuwa wakishinikiza kutimuliwa kwa Kasisi Ntombura pia wamefukuzwa.

"Kamati Kuu ya Kanisa la Methodist ingependa kufahamisha Wakenya, waumini na ummam, kuwa watu hawa na washirika wao ambao wanadai ni viongozi wa kanisa hilo wametumuliwa na hawaruhusiwi kushughulikia suala lolote kuhusu kanisa hili," ikasema notisi hiyo.

Hata hivyo, Askofu Kanyari na mrengo wake wamepuuza hatua hiyo wakisema haikuafikiwa kwa kufuata kanuni za kanisa.

NAIROBI

# Mradi kuajiri wanawake 100 kila mwaka

NA KNA>> **WANAWAKE** wasiopungua 100 wanatazamiwa kupatiwa mafunzo na kuajiriwa kila mwaka kupitia mpango wa ajira kwa wanawake unaofahamika kama 'Women on Wheels (WoW)' uliozinduliwa jana Jijini Nairobi.

Mpango huo ni sehemu ya Miradi ya Ustawishaji ya Kampuni ya Bamburi Cement chini ya Utofauti, Usawa na Ujumuishaji (DEI), na ngome za Afya, Usalama na Mazingira.

ELDORET

# Ahukumiwa kifo kwa kuua watoto watatu

TITUS OMINDE NA NEEMA CHEROTICH>> **MAHAKAMA** ya Eldoret imemhukumu kifo mwanamume aliyeshtakiwa kwa mauaji ya watoto watatu wa kakake, miaka mitano iliyopita.

Wakati wa kutolewa kwa hukumu hiyo hakuna jamaa yeyote wa familia ya mshukiwa alifika kortini.

Enock Onzanse, 33, alishtakiwa kwa kosa la kuwaua watoto wa ndugu yake mkubwa, James Ratemo Nyambane.